**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO**

**MUHTASARI WA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA MANISPAA TAREHE 31/10/2019**

**Wajumbe waliohudhuria**:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Pascal M. Kihanga | __ | Mstahiki Meya – Mwenyekiti |
| 2. | Ndg. Sheilla E. Lukuba | __ | Mkurugenzi wa Manispaa – Katibu |
| 3. | Mhe. Sengo Isiaka Mtandikile | __ | Naibu Meya – Mjumbe |
| 4. | Mhe. Hamisi Mohamed Msasa | __ | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Suzana Paulo Mtikwa | __ | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Wenslaus Kalogeries | __ | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Hassan Maringo | __ | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Gabriel M. Temba | __ | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Mizambwa R. Lugonzo | __ | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Samwel Msuya | __ | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Zahara S. Kitima | __ | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Dorothy J. Mwamsiku | __ | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Dismas Winfred Makanjira | __ | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Hadija Kombo Kibati | __ | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Spear A. Komanya | __ | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Zawadi Mohamed Kidando | __ | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Kifimbo Suddi Jumanne | __ | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Mudhihiri S. Shoo | __ | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Latifa Said Ganzel | __ | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Mabula Lusewa | __ | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Ally Rashid Kalungwana | __ | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Daud Salum Mnadi | __ | Mjumbe |
| 23. | Mhe. Zinduna Kombo Selemani | __ | Mjumbe |
| 24. | Mhe. Zamoyoni Juma Abdallah | __ | Mjumbe |
| 25. | Mhe. Peter Joel Dhahabu | __ | Mjumbe |
| 26. | Mhe. Tunda Amin Abdallah | __ | Mjumbe |
| 27. | Mhe. Amiri Juma Nondo | __ | Mjumbe |
| 28. | Mhe. Rashid R. Matessa | __ | Mjumbe |
| 29. | Mhe. Juma Abdu Tembo | __ | Mjumbe |
| 30. | Mhe. Amina H. Zihuye | __ | Mjumbe |
| 31. | Mhe. Hamisi A. Kilongo | __ | Mjumbe |
| 32. | Mhe. Gilbert Barnabas Mtafani | __ | Mjumbe |
| 33. | Mhe. Warda O. Bazia | __ | Mjumbe |
| 34. | Mhe. Castory Carlos Ndulu | __ | Mjumbe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 35. | Mhe. Scolastica William Mkude | __ | Mjumbe |
| 36. | Mhe. Milikiel Mansuet Mahiku | __ | Mjumbe |
| 37. | Mhe. Hilda Benedict John | __ | Mjumbe |

**Wajumbe wasiohudhuria**:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Abdulazizi Mohamed (Mb) | __ | Mjumbe |
| 2. | Mhe. Dr. Christine Ishengoma (Mb) | __ | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Devotha Minja (Mb) | __ | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Madaraka S. Bidyanguze | __ | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Kulthum Isaack Mwisongo | __ | Mjumbe |

**Waalikwa waliohudhuria**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Regina R. Chonjo | __ | Mkuu wa Wilaya ya Morogoro |
| 2. | Mhe. Fikiri H. Juma | __ | Mwenyekiti wa CCM Wilaya |
| 3. | Ndg. Leopold Ngirwa | __ | Mkaguzi wa Ndani Serikali za Mitaa Mkoa. |

**Watendaji waliohudhuria**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Michael W. Joseph | __ | Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika wa Manispaa |
| 2. | Ndg. Abdul Buhety | __ | Afisa Elimu Msingi wa Manispaa |
| 3. | Ndg. Winfred A. Kipako | __ | Afisa Tarafa wa Manispaa |
| 4. | Ndg. Neema Michael | __ | Mkaguzi wa Ndani wa Manispaa |
| 5. | Ndg. Upendo Elias | __ | Mratibu wa Kudhibiti UKIMWI wa Manispaa |
| 6. | Ndg. Feliciana Katemana | __ | Kny: Afisa Maendeleo na Ustawi wa Jamii wa Manispaa |
| 7. | Ndg. Dominica Ngaleka | __ | Kny: Afisa Utumishi wa Manispaa |
| 8. | Dr. Ikaji Z. Rashid | __ | Mganga Mkuu wa Afya wa Manispaa |
| 9. | Ndg. Safari A. Makupula | __ | Afisa Ununuzi na Ugavi w Manispaa |
| 10. | Ndg. Rumisha B. Kisanga | __ | Kaimu Afisa Mazingira na Udhibiti wa Taka Ngumu wa Manispaa |
| 11. | Ndg. Frank E. Mwago | __ | Kaimu Afisa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano wa Manispaa |
| 12. | Ndg. Enedy O. Mwanakatwe | __ | Afisa Maendeleo, Ustawi wa Jamii na Vijana wa Manispaa |
| 13. | Ndg. Patrick Sijapenda | __ | Afisa Usafirishaji wa Manispaa |
| 14. | Dkt. Janeth Barongo | __ | Afisa Elimu Sekondari wa Manispaa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 15. | Ndg. Salome Lyimo | __ | Kaimu Afisa Mipangomiji na Mazingira wa Manispaa |
| 16. | Ndg. Rehema Adam | __ | Mdhibiti Mkuu wa Ubora wa Shule Manispaa. |
| 17. | Eng. Juma Gwisu | __ | Kaimu Mhandisi wa Ujenzi wa Manispaa |
| 18. | Ndg. Elineema W. Mtaita | __ | Katibu TSC wa Manispaa |
| 19. | Ndg. Ponceano Kilumbi | __ | Mweka Hazina wa Manispaa |
| 20. | Ndg. Wilfred Mramba | __ | Mwanasheria wa Manispaa |
| 21. | Ndg. Ruben E. Urasa | __ | Mchumi |
| 22. | Ndg. Mohamed M.O. Chamzhim | __ | Afisa Mifugo na Uvuvi wa Manispaa |
| 23. | Eng. Benard Bwire | __ | Kny: Mhandisi wa Maji wa Manispaa |
| 24. | Ndg. Ziada E. Mallya | __ | Mchumi |
| 25. | Ndg. Alex Roman | __ | Afisa Mazingira |
| 26. | Ndg. Rutaihwa John | __ | Afisa Maendeleo ya Jamii |
| 27. | Ndg. Safia Kingwahi | __ | Afisa Utamaduni wa Manispaa |
| 28. | Ndg. Malambughi J.B. | __ | Afisa Elimu Taaluma Sekondari |
| 29. | Ndg. D.P. Mhaiki | __ | Afisa Elimu Taaluma Sekondari |
| 30. | Eng. Mnene James | __ | Meneja wa TARURA wa Manispaa |
| 31. | Ndg. Bariki J. Marandu | __ | Mhasibu |

**Sekretarieti:-**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Daudi A. Kibwana | __ | Katibu wa Mikutano |
| 2. | Ndg. Theresia Mbena | __ | Katibu wa Mikutano |
| 3. | Ndg. Sylvia Kahitwa | __ | Katibu wa Mikutano |
| 4. | Ndg. Maria R. Leke | __ | Katibu wa Mikutano |
| 5. | Ndg. Deogratias Butabile | __ | Katibu wa Mikutano |
| 6. | Ndg. Lilian K. Henerico | __ | Afisa Habari |

HMM/BM/21/ 2019/2020 Kufungua Mkutano

Kabla ya kufungua Mkutano, Mstahiki Meya aliwaongoza Wajumbe kuimba wimbo wa Taifa na Dua ya kuiombea Halmashauri.

Mstahiki aliwakaribisha Wajumbe na alifungua Mkutano saa 4:40 asubuhi.

HMM/BM/22/ 2019/2020 Kuridhia agenda za

Baraza la Madiwani liliridhia agenda za Mikutano zifuatazo:-

1. Kufungua Mkutano.
2. Maswali ya papo kwa papo kwa Mstahiki Meya na Mkurugenzi wa

Mkutano

Manispaa ya Morogoro.

3. Kusoma na kuthibitisha Mihtasari ya Mikutano ya Baraza la Madiwani ya tarehe 18/07/2019 (Mkutano wa mwaka), tarehe 31/07/2019 (Mkutano wa kawaida) na tarehe 16/09/2019 (maalum).

4. Yatokanayo na Mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani wa tarehe 31/07/2019.
5. Taarifa za Kamati za kudumu na Kamati nyinginezo za Halmashauri.

5.1 Kamati ya Fedha na Uongozi vikao vya tarehe 25/07/2019 (kawaida), tarehe 15/08/2019 (Kawaida), tarehe 11/09/2019 (Maalum), tarehe 16/09/2019 (kawaida), tarehe 27/09/2019 (dharura) na tarehe 04/10/2019 (Dharura).

5.2 Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya kikao cha kawaida cha tarehe 22/07/2019.

5.3 Kamati ya Mipangomiji na Mazingira kikao cha kawaida cha tarehe 23/07/2019.

5.4 Kamati ya Kudhibiti UKIMWI Kikao cha kawaida cha tarehe 24/07/2019.

5.5 Kamati ya Maadili ya Madiwani.

6. Uteuzi wa wawakilishi wa wananchi katika Bodi ya nane ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Manispaa ya Morogoro.
7. Kufunga Mkutano.

HMM/BM/23/2019/2020
Maswali ya papo kwa papo kwa Mstahiki Meya na Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro

**Kuhusu ujenzi wa Soko Kuu na ufukuaji wa Mto Kikundi:-**

Mjumbe mmoja alipongeza kwa hatua zilizochukuliwa na Halmashauri za kufukua Mto Kikundi ili kuepusha mafuriko katika Soko na Makazi ya watu nyakati za mvua na alisisitiza usimamizi mzuri uwepo kwa mkandarasi ili kazi hiyo ifanyike kwa ufanisi na kwa wakati.

**Swali:-**

Mjumbe alitaka kujua ujenzi wa Soko Kuu utakamilika lini?

**Jibu:-**

Ilielezwa kuwa Mkandarasi aliongezewa muda na ujenzi unatarajiwa kukamilika 31 Desemba, 2019.

HMM/BM/24/ 2019/2020 Kusoma na kuthibitisha Mihtasari ya Mikutano ya Baraza la Madiwani ya tarehe 18/07/2019 (Mkutano wa mwaka) , tarehe 31/07/2019 (Mkutano wa kawaida) na tarehe 16/09/2019 (maalum).

Mihtasari haikuwa na masahihisho hivyo ilithibitishwa kwa kusainiwa na Mwenyekiti na Katibu kuwa kumbukumbu sahihi za Mikutano.

HMM/BM/25/ 2019/2020 Yatokanayo na Mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani wa tarehe 31/07/2019

**1.0 Kuhusu choo katika Bustani ya Sabasaba.**

**Azimio**

Baraza liliafiki mapendekezo na lilielekeza kuwa Mkurugenzi wa Manispaa aweke mpango wa muda mfupi wa kujenga choo cha kawaida cha kulipia na mpango wa muda mrefu uwe ni kupendekeza aina ya Kitega Uchumi katika eneo hilo

**Utekelezaji**

Mchoro na BOQ zilishaandaliwa ziko katika hatua ya kutangazwa

**2.0 Kuhusu taarifa ya mdau aliyejitokeza kutoa mabati kwa Shule nne zenye vyumba viwili vya madarasa**

**Azimio**

Waheshimiwa Madiwani waliwasilisha maombi yafuatayo:-

- Shule ya Msingi Mafiga iliezuliwa ina mahitaji ya mabati.
- Shule ya Msingi Mkwajuni ina mahitaji ya kuezekwa vyumba Viwili.
- Shule ya Msingi Luhungo kuna darasa moja la awali linahitajika kupauliwa na kuezekwa.
- Shule ya Msingi Muungano Kata ya Mafisa ina mahitaji ya kuezekwa vyumba vya madarasa.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mstahiki Meya na Mkurugenzi wa Manispaa wakakague maombi yaliyowasilishwa na wafanye maamuzi.

**Utekelezaji**

Shule za Msingi Mkwajuni na Muungano zimepata fedha za ukamilishaji wa maboma kupitia EP4R na madarasa hayo yamekamilika. Aidha Halmashauri haitambui uwepo wa darasa la awali linalohitaji kupauliwa shule ya Msingi Luhungo.

**3.0 Kuhusu Kamati za Kudhibiti UKIMWI za Kata na Mitaa**

**Azimio**

Ilielezwa kuwa Kamati za Kudhibiti UKIMWI za Kata na Mitaa hazipo hai. Baraza lilielekeza kuwa Menejimenti itoe mafunzo ili ziwe hai.

**Utekelezaji**

Fedha za kuendesha mafunzo kwa Kamati za UKIMWI za Kata na Mitaa zitatengewa bajeti ijayo ya 2020/2021.

**4.0 Kuhusu ujenzi wa Soko Kuu**

Mjumbe mmoja aliuliza kuwa Mkataba wa ujenzi wa Soko Kuu ujenzi ulikuwa ukamilike tarehe 30 Septemba, 2019 lakini mpaka tarehe 31 Oktoba, 2019 haujakamilika. Mjumbe mtoa hoja alitaka kujua hatua alizochukuliwa Mkandarasi kwa kucheleweshe kazi.

**Ufafanuzi**

Ilielezwa kuwa hoja hiyo pia ilijitokeza kwenye kikao cha Kamati y a Fedha na Uongozi cha tarehe 21/10/2019, hivyo taarifa itawasilishwa na Kamati hiyo kwenye mkutano ujao wa Baraza la Madiwani.

**5.0 Kuhusu kibali cha ujenzi wa mradi wa maji katika Kata za Magadu na Mindu:-**

Mjumbe mmoja alitaka kujua kibali cha ujenzi wa mradi wa maji katika Kata za Magadu na Mindu kitatolewa lini.

**Ufafanuzi**

Ilielezwa kuwa suala hilo linashughulikiwa na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Morogoro (MORUWASA).

## 6.0 Kuhusu hali ya barabara za Manispaa ya Morogoro

Mjumbe mmoja alieleza kuwa hali ya barabara katika Manispaa ya Morogoro kwa sasa hairidhishi.

Mjumbe mtoa hoja alitaka kujua TARURA wamechukua hatua gani kuzitengeneza.

### Ufafanuzi

Ilielezwa kuwa tangu kuanzishwa kwa TARURA mwaka 2017 imekuwa ikipata fedha kidogo hivyo kupelekea utekelezaji wa miradi kuwa ni kidogo. Aidha, Meneja wa TARURA alikiri hali ya barabara za Manispaa kuwa ni mbaya. Pia, alieleza kuwa katika mwaka wa fedha 2019/2020 Kata zifuatazo zinaendelea kutengenezewa barabara;

1. Kata ya Mindu
2. Kata ya Mji Mkuu
3. Kata ya Boma
4. Kata ya Mbuyuni
5. Kata ya Kihonda
6. Kata ya Kihonda Maghorofani
7. Kata ya Mazimbu
8. Kata ya Lukobe
9. Kata ya Mafisa
10. Kata ya Mkundi

### Mjadala na maagizo

(i) Baraza lilielekeza kuwa TARURA itakapopata fedha iweke katika vipaumbele katika matengenezo ya barabara.

(ii) Meneja wa TARURA awe anawasilisha taarifa ya matengenezo ya barabara kwenye vikao vya Halmashauri.

Aidha, Baraza lilipongeza TARURA na TANROADS kwa uwekaji wa taa katika barabara.

(iii) Baraza lilielekeza kuwa Meneja wa TARURA aangalie uwezekano wa kutengeneza barabara inayoelekea Zahanati ya Kilakala

HMM/BM/26/2019/2020 Taarifa za Kamati za kudumu na Kamati nyinginezo za Halmashauri.

**1.0 Kamati ya Fedha na Uongozi vikao vya tarehe 25/07/2019 (kawaida), tarehe 15/08/2019 (Kawaida), tarehe 11/09/2019 (Maalum), tarehe 16/09/2019 (kawaida), tarehe 27/09/2019 (dharura) na tarehe 04/10/2019 (Dharura).**

Taarifa iliwasilishwa, ilipokelewa na iliridhiwa na wajumbe.

**2.0 Kamati ya Huduma za Uchumi, Elimu na Afya kikao cha kawaida cha tarehe 22/07/2019.**

Taarifa iliwasilishwa na ilipokelewa.

**Mjadala na Maagizo**

**Kuhusu ujenzi wa choo katika mnada wa Mifugo Nanenane**

**Hoja**

Mjumbe mmoja alihoji ni lini ujenzi wa choo katika mnada wa Mifugo Nanenane utaanza.

**Ufafanuzi**

Ilielezwa kuwa tayari fedha **Tshs. 10,000,000.00** zilishatolewa na ujenzi umeanza.

**Kuhusu utekelezaji wa Miradi viporo:-**

**Hoja**

Mjumbe mmoja alitaka kujua Halmashauri ina mpango gani wa kumalizia miradi viporo.

**Ufafanuzi**

Ilielezwa kuwa miradi viporo itatekelezwa kadri fedha zitakavyopatikana. Aidha baadhi ya Kata zimepelekewa fedha jumla ya **Tshs. 39,700,000.00** kwa ajili ya umaliziaji ujenzi . Kata hizo ni kama ifutavyo:-

1. Magadu
2. Luhungo
3. Mafisa
4. Sabasaba
5. Kihonda na,
6. Mlimani

**Kuhusu ukarabati wa majengo mbalimbali ya Shule ya Sekondari ya Morogoro:-**

**Hoja**

Mjumbe mmoja aliipongeza Serikali Kuu kwa kutoa fedha zaidi ya **billion 1.4** za ukarabati wa majengo mbalimbali ya shule ya Sekondari ya Morogoro. Alihoji ukarabati utakamilika lini.

**Ufafanuzi**

Ilielezwa kuwa ukarabati umefikia **asilimia 99**.

Baada ya mjadala Baraza liliridhia taarifa.

## 3.0 Kamati ya Mipangomiji na Mazingira kikao cha kawaida cha tarehe 23/07/2019.

Taarifa iliwasilishwa, ilipokelewa na iliridhiwa na Wajumbe.

## 4.0 Kamati ya Kudhibiti UKIMWI Kikao cha kawaida cha tarehe 24/07/2019.

Taarifa iliwasilishwa na kupokelewa.

**Marekeisho**

Marekebisho yalifanyika katika ukurasa 181 wa kabrasha kipengele Na. 1.9 jedwali la Idadi ya Wazee waliotambuliwa ili kupewa vitambulisho vya matibabu kama ifuatavyo:-

| NA | IDADI YA WAZEE WALIOTAMBULIWA | | JUMLA | WALIOPATA VITAMBULISHO | | JUMLA | IDADI YA MABARAZA YA KATA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | KE | ME | | KE | ME | | |
| | 7,294 | 6,674 | 13,968 | 2,481 | 1,521 | 4,002 | 29 |

Baada ya masahihisho hayo Baraza liliridhia taarifa.

## 5.0 Maadili ya Madiwani:-

Taarifa iliwasilishwa, ilipokelewa na kuridhiwa na Wajumbe.

HMM/BM/27/ 2019/2020 Uteuzi wa wawakilishi wa wananchi katika Bodi ya nane ya mamlaka ya maji safi na usafi wa mazingira Manispaa ya Morogoro.

Ilielezwa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro imepokea barua yenye Kumb. Na. CFA 288/547/0IC/19 ya tarehe 02 Oktoba, 2019 kutoka Wizara ya Maji yenye taarifa ya kuvunjwa kwa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA).

Aidha katika barua hiyo na kwa kuzingatia Sheria ya Maji Na. 5 ya mwaka 2019 kifungu Na.10 (2), Waziri wa Maji kwa mamlaka aliyopewa aliagiza Mstahiki Meya apendekeze majina matatu (3) katika Mkutano wa Baraza la Madiwani ambapo ni lazima Wajumbe wawe na elimu nzuri ya kuanzia kidato cha nne na wawe na uelewa mpana wa masuala ya maji yakiambatishwa na wasifu wao (CV) ili yawasilishwe kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro kabla ya tarehe 31/10/2019 ili ayawasilishe Wizara ya Maji kwa hatua zaidi.

**Mapendekezo**

Kwa mamlaka aliyopewa, Mstahiki Meya aliwapendekeza Waheshimiwa Madiwani wafuatao wawe wawakilishi katika Bodi ya Nane ya Mamlaka ya maji safi na usafi wa mazingira Manispaa ya Morogoro.

**Waliopendekezwa ni**

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Mhe. Hamisi Mohamed Msasa | ME |
| 2 | Mhe. Latifa Said Ganzel | KE |
| 3 | Mhe. Samwel Alfred Msuya | ME |

**Maamuzi:-**

Baraza la Madiwani liliridhia Wajumbe waliopendekezwa hapo juu wawe wawakilishi wa wananchi katika Bodi ya Nane ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Manispaa ya Morogoro kwa hatua zaidi.

HMM/BM/28/ 2019/2020 Kufunga Mkutano

Kabla ya kufunga Mkutano Mstahiki Meya alimpa fursa Mkuu wa Wilaya ya Morogoro ili atoe salaamu za Serikali.

**Salaamu za Mkuu wa Wilaya ya Morogoro.**

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro alimuomba Mstahiki Meya awe anampa nafasi mwanzoni mwa Mkutano ili aweze kuongea na Waheshimiwa Madiwani, Watendaji na Wananchi kusudi apate muda wa kufanya majukumu mengine ya Serikali

Alimpongeza Ndg. Sheilla E. Lukuba - Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro kwa kuteuliwa na alimkaribisha Manispaa ya Morogoro na aliwaomba Madiwani na Watendaji pamoja na wananchi wote wampe ushirikiano katika kutekeleza majukumu yake.

Baada ya salaamu hizo, Mkuu wa Wilaya aliongea yafuatayo;

**1.0 Kuhusu mradi wa ujenzi wa stendi ya Daladala Mafiga**

Alielekeza kuwa kila mradi unaotekelezwa kwenye Kata, Diwani wa Kata awe anapewa taarifa na kushirikishwa. Aidha, aliagiza Mkuu wa Wilaya awe anapewa andiko la mradi. Alifafanua kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro inajenga stendi ya Daladala katika Kata ya Mafiga lakini hajapewa taarifa ya mradi huo.

Aidha, alieleza kuwa gharama za ujenzi ya stendi hiyo ya **Tshs. 5,247,300,000.00** ambapo stoo inajengwa kwa **Tshs. 49,000,000.00**, vyoo **Tshs. 240,000,000.00** na jengo la utawala **Tshs. 450,000,000.00** ni kubwa hivyo aliagiza Wataalamu wapitie upya BoQ ili kuwepo na uhalisia wa thamani ya fedha.

**Maagizo**

i) Alimuagiza Mhandisi wa Ujenzi wa Manispaa na Meneja wa TARURA wa Manispaa wapitie upya gharama za ujenzi na mkataba ili kupunguza gharama za ujenzi na kazi hiyo iweze kukamilika tarehe 31/12/2019 badala ya mwezi Mei, 2020 kama ilivyoelekeza Serikali.

**Ii) Kuhusu kutumia Force Account katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo;** Alishauri kuwa miradi mingine ya Maendeleo itumike Akaunti hiyo kwa kuwa inapunguza gharama.

**2.0 Kuhusu mradi wa ujenzi wa Soko Kuu:-**

Alieleza kuwa mradi huo awali ulikuwa ukamilike mwezi Septemba, 2019 lakini Mkandarasi aliongezewa muda hadi tarehe 31/12/2019. Alielekeza kuwa Mkurugenzi wa Manispaa akaongee na Mkandarasi ili ajenge mchana na usiku ili mradi ukamilike mapema.

**3.0 Kuhusu Shule ya Sekondari Mjimpya**

Alieleza kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI atakuja kuifungua Shule hiyo hivyo alielekeza aombwe ili shule hiyo iwe ya kidato cha tano na sita.

Aidha iliagizwa kuwa Halmashauri iweke mipango kwenye Bajeti ijayo ili kujenga Shule mpya na siyo kuongeza katika Shule za zamani au kujenga kwenye viwanja vya michezo.

## 4.0 Kuhusu wananchi wa Kata ya Lukobe na Kilakala kuandamana kwenda kwa Mkuu wa Wilaya:-

Alieleza kuwa wananchi wa Kata ya Lukobe waliandamana katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya wakilalamikia Diwani wa Kata haonekani katika eneo lake la Utawala. Aidha wananchi wa Kata ya Kilakala wanamlalamikia Diwani wa Kata hiyo kutokushiriki vikao vya Baraza la Maendeleo la Kata. Hivyo alishauri wawepo kwenye Kata kuwahudumia wananchi na wahudhurie vikao vya Mabaraza ya Maendeleo ya Kata.

Baada ya maagizo hayo Mstahiki Meya aliyapokea na aliahidi kuyasimamia kwa utekelezaji.

Mstahiki Meya aliagiza kuwa ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo ufanyike hususani ujenzi wa stendi ya Daladala ya Mafiga.

Alifunga mkutano saa 6:15 mchana.

Muhtasari umethibitishwa tarehe .....

| | |
|---|---|
| ..... | ..... |
| Mhe. Pascal M. Kihanga | Ndg. Sheilla E. Lukuba |
| Mstahiki Meya | Mkurugenzi Wa Manispaa |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |

**YATOKANAYO NA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA WA TAREHE 31/10/2019**

| MUHT. NA | AZIMIO | MTEKELEZAJI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| HMM/BM/25/ 2019/2020 Yatokanayo na Mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani wa tarehe 31/07/2019 | **1.0 Kuhusu hali ya barabara za Manispaa ya Morogoro**<br>**i)** Meneja wa TARURA awe anawasilisha taarifa ya matengenezo ya barabara kwenye vikao vya Halmashauri. | Meneja wa TARURA | TARURA Manispaa itakuwa inawasilisha taarifa zake kwenye vikao vya Halmashauri kama ilivyoelekezwa. |
| | **ii)** Baraza lilielekeza kuwa Meneja wa TARURA aangalie uwezekano wa kutengeneza barabara inayoelekea Zahanati ya Kilakala. | Meneja wa TARURA | TARURA Manispaa ya Morogoro itaweka kwenye bajeti zake za matengenezo ya barabara ambazo zinaelekea kwenye maeneo ya huduma muhimu za kijamii na fedha zikipatikana barabara hiyo itajengwa. |
| HMM/BM/28/ 2019/2020 Kufunga Mkutano | **2.0 Kuhusu mradi wa ujenzi wa Stendi ya Daladala Mafiga**<br>**i)** Mhandisi wa Ujenzi wa Manispaa na Meneja wa TARURA wa Manispaa wapitie upya gharama za ujenzi na mkataba ili kupunguza gharama za ujenzi na kazi hiyo iweze kukamilika tarehe 31/12/2019 badala ya mwezi Mei, 2020 kama ilivyoelekeza Serikali. | Meneja wa TARURA | Ushauri ulizingatiwa na kufanyiwa kazi kupitia maeneo ambayo yataondolewa pasipo kuathili utekelezaji wa mradi huo. Benki ya Dunia kupitia kikao kilichofanyika Dar es Salaam kuanzia tarehe 10-13/12/2019 walitoa maelekezo kwa mradi wa ULGSP utafungwa rasmi mwezi Juni, 2020. Mkandarasi anaendelea na utekelezaji ambapo matarajio ni kukamilisha mradi kabla ya muda wa mkataba. |